JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

Shule ya Sekondari Makanya
S. L. P 114,
SAME.
15/12/2020

MZAZI/MLEZI WA …….

YAH: KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAKANYA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii kwa mwaka wa masomo 2021. Muhula wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021** unashauriwa kuripoti siku hiyo kwa usajili na mwisho wa usajili itakuwa tarehe **18/01/2021.**

Mambo muhimu ya kuzingatia.

1.0 Sare ya Shule.

1.1 Sare yako ya shule itakuwa ni suaruali mbili rangi ya **DAMU YA MZEE**(MAROON) na mashati mawili meupe (Tomato) ya mikono mifupi kwa upande wa wavulana, na sketi ndefu mbili rangi ya **DAMU YA MZEE** (MAROON) na mashati mawili meupe (Tomato) kwa wasichana ya mikono mifupi.

1.2 Kwa wanaovaa Hijabu iwe nyeupe na isiwe na urembo.

1.3 Soksi ndefu (stoking) nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana

1.4 Viatu nyeusi vya ngozi vinavyofunika miguu vyenye kisigino kifupi na vya kufunga kwa kamba.

Muundo wa Mashono ya sare.

(a) Suruali: Ziwe pana sio modal na ziwe na marinda mawili mbele. Ziwe na upana wa kutosha kwa chini na ziwe na “turn up” .

(b) Sketi : Ziwe na marinda mapana kwa mbele na nyuma na marinda madogo madogo ubavuni. Zisiwe na mkanda mpana (kantangaze) ziwe ndefu na zisibane.

2.0 Mahitaji mengine

Edit with WPS Office

2:1 Madaftari makubwa 10 Counter Book Quire 3, kalamu za wino nyeusi/bluu, penseli na mkebe (mathematical set) rula na vifaa vingine vya darasani.

2:2 Sahani ya bluu, kikombe cha bluu cha nusu lita na kijiko kwa ajili ya chakula na uji.

3 Vifaa vya usafi

3.2 Wavulana wote kila mmoja alete jembe **jipya** na mpini wake na fagio kubwa la kufagilia.

3.3 Wasichana wote kila mmoja alete ndoo ya lita 10 na fekeo.

.

4.0 Sheria na Kanuni za Shule.

Shule inaongozwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha tunazingatia miongozo yote iliyotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

4.1 Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenyewe na jamii kwa ujumla ni muhimu.

4.2 Mahudhurio mazuri katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa .

4.3 Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako hapa shuleni.

4.4 Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule wakati wote

4.5 Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

4.6 Kuzingatia kikamilifu ratiba ya shule wakati wote.

4.7 Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa

5.0 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ufukuzwe shule

5.1 Wizi

5.2 Uasherati na Ushoga

5.3 Ubakaji

5.4 Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kuberi n.k

5.5 Kupigana au kupiga

Edit with WPS Office

5.6 Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

5.7 Kudharau Bendera ya Taifa

5.8 Kuoa au kuolewa

5.9 Kupata mimba au kuharibu (kutoa) mimba ndani na nje ya shule

5.10 Kugoma kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule

5.11 Kukataa adhabu kwa makusudi

5.12 Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

6.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.

6.1 “Medical Examination form” iliyoambatanishwa ijazwe baada ya kupimwa na mganga Mkuu wa hospitali ya serikali au kituo cha Afya. Ikabidhiwe kwa Mkuu wa shule mara utakapo ripoti shuleni. NB: Mzazi kama mwanao ana tatizo lolote la kiafya usisite kuliweka wazi ili na sisi tumwekee mazingira mazuri ya kumlea.

6.2 Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi .

7.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MAKANYA.

Wenu,

…….

BERNARD F MGAYA

MKUU WA SHULE

Edit with WPS Office

HALMASHAURI YA WILIYA YA SAME
SHULE YA SEKONDARI MAKANYA
MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

JAZA KIKAMILIFU NA KWA USAHIHI

1. Jina kamili la mwanafunzi ……Me ( ) K e ( )Weka **(√)** panapostahili.
2. Tarehe na mwaka wa kuzaliwa……..
3. Shule ya Msingi uliokotoka ……
4. Jina kamili la mzazi/mlezi …….
5. Anuani ya mzazi/ mlezi ……..

WEKA (√) PANAPOSTAHILI.

6. Yatima, NDIO ( ) HAPANA ( ), mzazi mlezi mmoja ( ) wawili ( ) Eleza kuwa ni baba/mama au wote wawili ……
7. Anaye husika kukusomesha :
   Jina kamili ……..Uhusiano/undugu ……..
   Kazi yake …… … Sekta/Taasisi itaje ……..

Mimi ……ninakubali kuchaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule ya Makanya Sekondari mwaka 2021
Ninaahidi kuwa nitajitahidi kwa uwezo wangu wote na kutii sheria zote za shule. Sitaleta usumbufu wa aina yoyote kwa mzazi/mlezi wala uongozi wa shule.
Sahihi ya mwanafunzi …… Tarehe …….
Mimi …… mzazi/mlezi wa mwanafunzi ……
Nina ahidi kugaramia mahitaji yote muhimuya shule na sitomkosesha haki yake na elimu na pia sitaleta usumbufu wa aina yoyote kwa uonogozi wa`shule.
Sahihi ya mzazi/mlezi …… Tarehe …….

NB: Tafadhali uje na form hii ikiwa imejazwa kikamilfu
Nakutakia utelezaji mwema

……
BERNARD F. MGAYA
MKUU WA SHULE.

Edit with WPS Office

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA`MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

Simu +255272759901
Barua pepe makanya.sekondari@gmail.com
Kumb. Na MSS/F.1/FS/ …….

Makanya Sekondari
S. L. P 114
Same
15/12/2020

Mganga Mkuu (W)
Kituo cha Afya
……
……

YAH: MWANAFUNZI KIDATO CHA I MWAKA 2021

Rejea somo tajwa hapo juu

Ninaomba utusaidie kumfanyia uchunguzi mtajwa hapo juu kisha utujazie sehemu husika hapo chini. Natanguliza Shukrani.

……
Mkuu wa Shule

Tafadhali tumia alama **(✓) sehemu ya** Ndio au **(X)** sehemu ya Hapana.

i. Kifafa Ndio …… Hapana……
ii. Moyo Ndio ……. Hapana…….
iii. Ukisoefu wa damu (Anemia/sickle sell) Ndio ……Hapana……..
iv. Pumu Ndio …… Hapana……
v. Kisukari Ndio ……Hapana ……
vi. Vidonda vya tumbo Ndio ……Hapana ……
vii. Kichocho Ndio …….. Hapana ……..
viii. Malaria sugu Ndio ……. Hapana ……
ix. Magonjwa ya zinaa Ndio …….. Hapana …….
x. Ujauzito Ndio ……. Hapana …….
xi. Je ana dosara nyingine yoyote ya kiafya?. **ITAJE** (Mfano: Macho, masikio au ulemavu mwingine).

……
……
……

Edit with WPS Office

……

Jina ……..

Muhuri

Edit with WPS Office